OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA TARIME

SHULE YA SEKONDARI ITIRYO,
S. L. P 99,
TARIME.

Kumb. Na. HWT/ITR/SS/F1.2021

JINA LA MWANAFUNZI_____

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI ITIRYO, WILAYA YA TARIME MKOA WA MARA 2021

1.0. UTANGULIZI:

Ninafuraha kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika Shule ya Sekondari Itiryo mwaka 2021. Shule ya Sekondari Itiryo ipo umbali wa Km 40 mashariki mwa mji wa Halmashauri ya Wilaya ya Tarime. Usafiri wa magari kutoka Tarime mjini unapatikana katika kituo cha mabasi cha Tarime na nauli ni Tsh 5,000/-. Muhula wa kwanza masomo utaanza tarehe 11/01/2021, unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 11/01/2021 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 16/01/2021 ndani ya siku tano. Baada ya siku hizo kupita ambao watakuwa hawajaripoti watatafutwa walipo na kuchukuliwa hatua kali za kisheria.

2.0. Mambo muhimu ya kuzingatia.

2.1. Sare za Shule

❖ WASICHANA

1. Sketi mbili (2) Bluu Bahari na Karoti/Orange za marinda box, za marinda sita (6). Rinda tatu kushoto na rinda tatu kulia. Sketi zivuke magoti.
2. Blauzi mbili mikono mifupi, rangi nyeupe.
3. Viatu vya ngozi vyeusi vyenye visigino vifupi.
4. Nguo za michezo na viatu vya michezo (tracksuits blue bahari na raba rangi nyeusi)
5. Sweta ya kijivu lenye "V" shingoni.
6. Soksi nyeupe ndefu
7. Watakaovaa hijabu, hijabu ifanane na sare za shule

❖ **WAVULANA**

1. Suruali mbili (2) Bluu bahari na Jani la mgomba zenye mifuko mitatu na ziwe na marinda manne, mawili kushoto na mawili kulia, tanapu ya kukunja, na upana wa chini wa suruali uwe nchi 16 "**SURUALI MODO HAZITAKIWI SHULENI)**.
2. Shati mbili zenye mikono mifupi, rangi nyeupe.
3. Viatu vya ngozi vyenye soli fupi vinavyofunika miguu, rangi nyeusi.
4. Soksi nyeusi zisizokuwa na madoadoa.
5. Sweta rangi ya kijivu lenye "V" shingoni.
6. Nguo za michezo na viatu vya michezo (tracksuit blue bahari na raba rangi nyeusi)

NB: VITAMBAA VYA KUSHONA SARE YA SHULE (SURUALI NA SKETI) VIWE GREDI YA KWANZA (No 1) UTAPATA MAELEKEZO ZAIDI SHULENI.

2.2. VIFAA VYA KUTUMIA DARASANI: - (Lazima mwanafunzi awe navyo)

1. Madaftari makubwa tisa (9). Na mngine madogo tisa ya mazoezi.
2. Mathematical set moja yenye vifaa vyote, rula moja yenye vipimo ya sm 30/futi moja.
3. Dictionary moja (Oxford English Dictionary) itakaguliwa siku ya kuripoti.
4. Begi la kubebea madaftari (school bag) mwanafunzi asije na mifuko ya plastiki/Rambo.

3.0. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na.10 ya mwaka 1995 ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia, na Mafunzo ya Ufundi yenye dhamana ya Elimu Nchini na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu.

Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala mara baada ya kuripoti shuleni.

a. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine, jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ya ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
c. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
d. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wanafunzi wawapo shuleni.
e. Kufanya usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
f. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
g. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
h. Kutunza mali za UMMA.

A: MAMBO AMBAYO MWANAFUNZI HARUHUSIWI KUFANYA KABISA.

A. Kutumia madawa ya kulevya na kuvuta sigara.
B. Kufuga kucha ndefu, nywele ndefu na kufuga ndevu.
C. Kuvaa mavazi yasiyo sare rasmi ya shule ndani ya eneo la shule muda na suku za shule.
D. Kumbana, kugombanisha au kufanya ugomvi/kuchochea mgomo.
E. Kuiga mitindo ya kihuni/isiyo faa, kama kuvaa milegezo, kuvaa nguo fupi (vimini) na vitopu, kuchora tatuumwilini n.k.
F. Kuchubua ngozi ya mwili kwa kutumia madawa.
G. Kwenda nje ya shule bila ruhusa muda wa vipindi na muda wowote uwapo shuleni.
H. Kuvaa kofia, bangili na mapambo mengine yasiyo sehemu ya sare ya shule.
I. Kuwa na simu, kamera na radio shuleni.
J. Kutembelewa na wageni muda wa vipindi.
K. Kukiuka RATIBA au utaratibu wa Shule.
L. Kutembelea maeneo yanayouza vileo/pombe na kunywa pombe.

B: MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE MARA MOJA NI: -

1. Wizi
2. Uasherati, Ubakaji, Ushoga na Usagaji.
3. Uvutaji Bangi na Sigara.
4. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya/mihadarati.
5. Makosa ya Jinai.
6. Kupigana/kupiga.
7. Kuharibu kwa makusudi mali ya Umma.
8. Kudharau Bendere na wimbo wa Taifa.
9. Kuoa/kuolewa.
10. Kusaidia kutoa mimba au kutoa mimba.
11. Kugoma, kuchochea na kuongoza fujo zenye kuvuruga Amani, usalama wa watu na mali ya Umma.
12. Kukataa adhabu kwa makusudi.
13. Kutoingia katika vipindi/darasani au kukataa kufanya mitihani na mazoezi.
14. Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi shuleni.

4.0. **MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI; -**

a. Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakaporipoti shuleni.
b. Fomu ya maelekezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo, na makosa ya jinai.
c. Fomu ya Mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.
d. Tafadhali soma kwa makini maelekezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA KATIKA SHULE YA SEKONDARI ITIRYO,

……..

PAULO MAGAIWA
SIMU: 0753604207/0623346863
MKUU WA SHULE

HALMASHAURI YA WILAYA YA TARIME
SHULE YA SEKONDARI ITIRYO

TARIFA YA MWANAFUNZI:

1. MAJINA KAMILI YA MWANAFUNZI: _____
2. MAJINA YA MZAZI/MLEZI _____
3. KAMA NI MLEZI: UHUSIANO_____ NAMBA ZA SIMU _____
4. ANWANI YA KUDUMU YA MZAZI/MLEZI _____
5. MAHALI MWANAFUNZI ALIPOZALIWA: KIJIJI _____ KATA _____ WILAYA _____ MKOA _____
6. DINI _____ DHEHEBU _____
7. KUTOKA SHULE YA MSINGI_____ WILAYA_____ MKOA_____
8. NDUGU WENGINE WANAOWEZA KUPELEKEWA TAARIFA ZAKO MUHIMU ZA MASUALA YA SHULE NI:
   I. _____ UHUSIANO _____ NAMBA SIMU_____
   II. _____ UHUSIANO _____ NAMBA SIMU_____
   III. _____ UHUSIANO _____ NAMBA SIMU_____
9. KABLA HUJARIPOTI SHULENI UMEPIMWA NA DAKTARI? NDIO/HAPANA. NI UGOJWA UPI NI WA KUDUMU KWAKO? _____
10. SIFA MAALUMU KAMA UNAZO/YO _____
11. TAARIFA ZA WAZAZI: WAPO _____ WALIFARIKI/ALIFARIKI _____ (weka alama ya vema panapohusika)

MAELEZO YALIYOPO HAPO JUU NI SAHIHI

_____ _____

SAHIHI YA MWANAFUNZI SAHIHI YA MZAZI/MLEZI

AHADI YANGU MIMI (Jina la Mwanafunzi) _____ nakubali kwa dhati kabisa nafasi hii niliyopewa na Taifa kujiunga na shule hii. Naahidi kuitumia nafasi hii vizuri kwa kuendelea na masomo haya mpaka nimalize kidato cha nne bila kuacha shule au bila kuwa mtoro sugu na naahidi kufuata sheria za Shule na taratibu zote kama zilivyotolewa na zitakavyotolewa na uongozi wa Shule, ikiwa ni pamoja na kutoshiriki katika migomo au fujo na makosa ya jinai.

MIMI MZAZI/MLEZI (Jina la Mzazi/Mlezi) _____ Nimeyasoma masharti, kanuni na sheria za Shule ya Sekondari Itiryo ambako kijana wangu amechaguliwa kujiunga. Naahidi kwamba nitamhimiza mwanangu kufuata sheria, kanuni na taratibu zote za Shule kama zilivyotolewa. Aidha naahidi kushirikiana na uongozi wa shule kuhakikisha mwanangu anaendelea na masomo mpaka amalize kidato cha nne na katika kutoa malezi bora kwa mwanangu ili baadae awe raia bora na mwema wa Taifa letu na kwa ulimwengu mzima.

Tarehe _____
Sahihi ya Mwanafunzi _____
Jina la Mwanafunzi _____

Tarehe _____
Sahihi ya Mzazi/Mlezi_____
Jina la Mzazi/Mlezi _____

PRESIDENT'S OFFICE
REGIONAL ADMINISTRATION, AND LOCAL GOVERNMENT
TARIME DISTRICT COUNCIL
MEDICAL EXAMINATION FORM

ITIRYO SECONDARY SCHOOL,
P. O. Box 99,
TARIME.

TO:
MEDICAL OFFICER
P. O. Box _____
_____
Dear Sir/Madam,

REF: **STUDENT'S MEDICAL EXAMINATION.**
(To be completed by Governmental Medical Officer)
Full Name _____
Age _____ Height (in cm) _____ Weight (in kgs)_____

1. Blood count _____ (Red/White) _____
2. Stool Examination _____
3. Urine Analysis _____
4. Syphilis and other V.D _____
5. T. B and Leprosy Test _____
6. Eye Test _____
7. Ear Test _____
8. Chest Test _____
9. Abdominal Test _____
10. Blood Group (very crucial) _____
11. Spleen _____
12. H. I. V Test, Positive _____ Negative _____ (Tick where necessary)
    Additional information e.g. Physical defects or impairments, infection, chronic of family Diseases like Sickle cell.
    _____
    _____
    _____
    _____
    _____
    I certify that the above student is fit/is not fit to pursue Secondary Education.

    Signature ……
    Designation……
    Station ……
    Date ……